Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 5, Issue 4

18th Muharram 1432

24th December, 2010

Yaliyomo

Uvumi Na Khatari Zake Katika Ummah 1 - 3

SUTRAH 3 - 4

UVUMI NA KHATARI ZAKE KATIKA UMMAH

Mtayarishi: Sheikh Dr. 'Abdul-Adheem Badawi [Al-Aswaalah]

Amesema Allaah (عز وجلّ) katika kitabu chake kitukufu: **"Enyi Mulioamini! Akiwajia nyinyi mtu asiyeaminika katika (kutoa Khabari) kwa Khabari yoyote fanyeni uchunguzi juu ya Khabari yake msije mkawadhuru watu kwa kutojua na mukapambaukiwa kwa muliyoyafanya ni wenye kujuta."** [al-Hujuraat: 6]

Anawakataza Allaah (سبحانه وتعالى) waja wake waumini juu ya kufuata Khabari za Uvumi na anawaamrisha kuthibitisha ukweli wa Khabari zinazoletwa kwao, kwani si kila kisemwacho huwa ni kweli. Na hakika ya maadui zenu wanawatafutia kila ndia ya kuwamaliza (kila upande). Kwahiyo, ni wajibu kwenu nyinyi kuwa macho siku zote ili mumjue yule anaetaka kuleta uchochezi na kueneza fitna, na kueneza uvumi ambao usokuwa na msingi swaheeh.

Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Enyi Mulioamini! Akiwajia nyinyi mtu asiyeaminika (katika kutoa Khabari) kwa Khabari yoyote fanyeni uchunguzi."** Yaani musiikubali Khabari yake mpaka iwabainikie nyinyi ukweli wake na muithibitishe ukweli wake na mupate ushahidi na huja za kweli zenye kuonyesha ukweli wa Khabari yake. Akatujuza Allaah (سبحانه وتعالى) yakwamba asli ya mtu faasiq ni kusema urongo lakini huwenda akawa mkweli (katika baadhi ya nyakati). Kwahiyo, haikubaliwi Khabari yake wala hairudishwi ila baada ya kuthibitishwa uswaheeh wa kauli yake. Ikibainika ukweli wake kwa dalili na ushahidi itakubaliwa khabari zake. Lau kama si hivyo itakuwa ni yenye kurudishwa (na kutokubaliwa). Kisha akataja Allaah (سبحانه وتعالى) lengo la kuimarisha kwake juu ya kuthibitisha jambo na ukatazo wa kufuatilia uvumi, akasema lengo lake **"musije mukawadhuru watu kwa kutojua."** Kisha likawabainikia nyinyi kosa lenu na kuwa mbali kwa yule aliyedhuriwa na mukapambaukiwa kwa muliyoyafanya ni wenye kujuta. Na khususan pindi zitakapokuwa zishawaumiza mboko kwenye migongo yenu. Kwa mfano endapo mulililoliingilia lilikuwa ni jambo ambalo lenye kuwapasa nyinyi kusimamishiwa haddi (hukmu ya kuchapwa) kama kumsingizia mtu. Kuna haja kubwa iliyoje kwa Waislamu wote kuijua aya hii waisome na waizingatie, na kujipamba na adabu zake. Kwani fitna ngapi zimetokea kwa Khabari za urongo zilizonukuliwa na mtu faasiq (muovu)? Damu ngapi zilizomwagwa, roho ngapi zilizotoka, mali ngapi zilizotwaliwa, heshima ngapi zilizovundwa kwa sababu za khabari za urongo zisizokuwa na msingi zilizoundwa na maadui wa ki-Islamu ili kuvunda umoja wao kwa khabari hizo, na kuvunda mashikamano yao na kueneza kati yao uadui na chuki? Mifarakano mingapi ilotokea baina ya ndugu wawili kwa sababu ya khabari za urongo? Mifarakano mingapi ilotokea baina ya mume na mke kwa sababu ya khabari za urongo? Ni Makabila mangapi yaliyopigana kwa sababu ya khabari za urongo na Allaah (عز وجلّ) ameuwekea Ummah huu msingi wa kisheriya ili kuuhifadhi Ummah huu na utengano na mafarakano na vilevile kuuhifadhi na kutowaka moto wa fitna kisha usiweze kuzimika milele.

Na miongoni mwa yenye kusikitisha ni kwamba hakukuwahi kukosekana ndani ya mujtama' miongoni mwa mujtama' za Waislamu wanafiki wenye vifundo na uhasidi ambao haiwafurahishi wao kuona mujtama' wa ki-Islamu ni mujtama' ambao uloshikamana, wenye undugu na kusaidiana na kuhurumiana pindi wapatwapo na misiba. Na ni waajib kwa Waislamu kutukuwa tahadhari, na wawe ni wenye kuzinduka kwa maadui zao, na wajue kuwa maadui zao wanakesha katika kupanga mipango yao na vitimbi juu yao, na ni wajibu kwa Waislamu wawe daima na tahadhari ili wapate kujua ni wapi panapoleta utesi na ni yapi yanayosababisha bughdha kati yao. Hakika kupatikana wanafiki katika mujtama' wa ki-Islamu ni jambo ambalo lenye kuleta khatari kubwa. Lakini la khatari zaidi ni kuweko watu miongoni mwa waumini wazuri wenye kuwakubalia wao (wanafiki) kila wanayowaambia. Na wanawafungulia masikio yao kwa kuyasikiza kila wanayowahadithia na huku wakiwafuata kwa nyuma yao kwa maneno na vitendo pasi na kujali. Hakika imetusajiliya sisi Qur'aan khabari ya majuto ambayo yaliyowapata Waislamu kwa sababu ya kutembea baadhi yao nyuma ya wanafiki wenye chuki na hasad. Ili tufaidike na majaribio ambayo yaliyowafika wale walokuwa kabla yetu, soma ukitaka (kujua) Suratun-Nur na uzingatie aya zenye baraka ambazo alozisema Allaah (عز وجلّ) katika kuwatakasa Mama zao Waumini. Bibi 'Aaisha (رضي الله عنها), kwa tuhma (uvumi) walomtuhumu nazo wanafiki, wakenda katika mwendo wao ule ule katika tuhma hii pasi na kuwa na ushahidi wala dalili kikundi cha watu miongoni mwa waumini wa kweli.

UVUMI NA KHATARI ZAKE KATIKA UMMAH

Katika tafsiri ya al-Baghawi (4/181): "Asema Allaah (سبحانه وتعالى): **'Hapana shaka waliokuja na uzushi muovu (kumsingizia bibi 'Aaisha uzinifu).'** [an-Nur: 11]. Yaani khabari za urongo (ndizo hizo 'IFQ') urongo mbaya. Zimeitwa 'IFQ' kwa sababu ni urongo wenye kumgeuza mtu kabisa katika haki. Bibi 'Aaisha (رضي الله عنها) alikuwa ni mwenye kustahiki sifa nzuri kwa sababu ya heshima na ubora alokuwa nazo mpaka ikawa yule alomsingizia uovu amegeuza mambo kutoka katika ndia yake ya ukweli." Aendelea kusema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Msiuzingatieni uzushi huu kuwa ni shari kwenu"** yaani msidhani yale yalosemwa kuwahusu nyinyi nyumba ya Abu Bakr ni shari kwenu (bali ni kheri kwenu) na kheri ya kwanza ni kule kukutajeni Allaah kwa viumbe vyake wa juu na akateremsha aya kuwahusu nyinyi zenye kusomwa. Na kuteremshwa aya hii iliwaondokea huzuni likaondoa giza la tuhma na kuondoa jabali la huzuni lililokuwa limeteremka kwenye moyo wa mama wa Waumini, bibi 'Aaisha (رضي الله عنها) na babake as-Siddiq kama ilivyomuondokea huzuni kwenye moyo wa Swahaba muamnifu aliyetuhumiwa Swafwaan Bin Mu'attwal (رضي الله عنه). Kisha zikaanza aya kuwafundisha Waumini namna ya kupambana na uvumi na vipi wataweza kupambana na urongo na warongo. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Mbona mliposikiya khabari hii wanaume Waislamu na wanawake, hawakuwadhania wenzao wema wakasema huu ni uzushi ulio wazi."** Hii ndiyo hatua ya kwanza inayokupasa ewe Muislamu kuichukuwa inapokufikilia khabari kuhusu ndugu yako ikiwa wewe ulikuwa ukimdhania vizuri na kuiweka mbali nafsi yako na yale yanayosemwa kuhusu ndugu yako. Basi itakuwa ni wajibu kwako kumdhani vizuri ndugu yako. Na ujiweke mbali (kutomdhania) na yale anayosemwa nayo. Na useme: "**Umetakasika Mola wetu, huu ni uwongo mkubwa."** [Surat an-Nur:16] yaani haiwezekani kwa ndugu yangu kusema haya au kufanya haya. Na hivi ndivyo walivyofanya baadhi ya maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakati yalipowafikia wao yale yaliyowafikia kuhusu mama yao Waumini, bibi 'Aaisha (رضي الله عنها).

Imepokewa kutoka kwa Abu Ayyub al-Answari yakwamba aliambiwa na mkewe: "Ewe Abu Ayyub, umeyasikiya yale wanayoyasema watu juu ya bibi 'Aaisha (رضي الله عنها)? Akasema; "Ndio na huwo ni urongo. Jee, wewe (Umm Ayyub), waweza kufanya kitendo kama kile?" akajibu, "Laa, Wallaahi siwezi kufanya hivyo." Akamwambia Abu Ayyub, "Basi Wallaahi, 'Aaisha (رضي الله عنها) ni bora kuliko wewe." [tafsiri Ibn Katheer 3/273].

Kisha akaendelea kusema Allaah (عز وجلّ): **"Basi mbona hawakuweka wazushi mashahidi wanne (wakashuhudia) na ikiwa hawakuwaweka mashahidi basi hao mbele ya Mola wao ni waongo."** Hii ni hatua ya pili ambayo ni wajibu kwa kila Muislamu kuichukuwa litakapomfikiya yeye kutoka kwa ndugu yake lenye kumtuhumu.

Khatua ya kwanza ilikuwa ni kutaka dalili kwa utondoti nayo ni kumdhania ndugu yako dhana nzuri. Khatua ya pili ni dalili ya kihisiya. Asema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Enyi Mulioamini! Akiwajia nyinyi mtu asiyeaminika (katika kutoa habari) kwa habari yoyote fanyeni uchunguzi."** Yaani takeni kutoka kwa yule atakaewajilia nyinyi na dalili na ushahidi juu ya ukweli wa lile alilokuja nalo. Akija na ushahidi wa kisawasawa zitakubaliwa khabari zake. Lau kama si hivyo atarudishiwa khabari zile kwa sababu ni faasiq, mrongo na wajizuiye watu wote kutukuwa khabari hizi za urongo ambazo hazina msingi wowote. Kwa ndia hii itakuwa ni wenye kufa na kumalizika habari za uvumi na kuzikwa kwenye vifuwa vya wale wenye kuueneza uvumi wakati watakapokosa wa kuzichukuwa habari zao na kuzikubali.

Na hivi ndivyo Qu'aan inavyowalea watu (kwa mafundisho kama haya) lakini la kusikitisha utaona wengi miongoni mwa Waislamu hawajifungamanishi na malezi haya. Kwa sababu haenezi mnafiki aliye hasidi na chuki khabari za urongo dhidi ya mmoja miongoni mwa Waislamu mpaka itakuwa ni yenye kuenea na kusambaa khabari ile katika mujtama' wote na kuzipokea ndimi za watu khabari zile pasi na kuthibitisha.

Na ndio Allaah (سبحانه وتعالى) akasema: **"Mulipoupokea urongo huu mkubwa mukautangaza kwa ndimi zenu."** [Surat an-Nur: 15]

Asli ya maneno hupokewa mwanzo na masikio, wala si ndimi. Lakini Allaah anaeleza namna ya haraka yalivyotukuliwa maneno yale na kuenezwa baina ya watu kanakwamba tamko latoka kutoka kwenye ulimi na kwenda kwenye ulimi. Pasi na kupita kwenye masikio yenye kupeleka maneno yale mpaka kwenye moyo ambao hufikiriya yale yaliyosikiya. Ili apate kufikiriya mwana-adamu baadae juu ya kufaa kutukuliwa maneno yale na kutofaa kutukuliwa. Akasema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na mnayasema musiyokuwa na hakika nayo."** Yaani wala hamuna dalili juu ya jambo hilo; **"Na mwadhania ni dhambi dogo na ilhali mbele ya Allaah ni madhambi makubwa."**

Na baada ya Allaah kuwafundisha Waumini adabu hizi na kuwafunza vipi watakavyokabiliana na uvumi na kujitahidi kwa kila ndia kuumaliza haliyakuwa bado ni mchanga ili usienee katika mujtama' baada ya hapo yuwatahadharisha Allaah Waumini na kuzama katika mambo ambayo hawana ujuzi nayo. Yuwatahadharisha na tabia ya kuwafuata na kuwasikiza warongo wenye kueneza uvumi na Propaganda. Yuasema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Yuwawapa Allaah mawaidha kuwa musirudie tena kwa kitendo kama kile milele, ikiwa nyinyi ni wenye kuamini."** [Surat an-Nur:17]

Kisha yuazidi kuwabainishiya Waumini kuwa tabia ya kuwafuata warongo wenye kueneza Propaganda ni kufuata mwenendo wa Sheitaan. Asema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Enyi Mulioamini! Musizifuate hatua za Sheitaan (mwenendo); na atakaefuata hatua za Sheitaan, basi hapana shaka yeye Sheitaan yuaamrisha uovu na uchafu,"** [Suurat an-Nur:21]. Kisha yuabainisha kuwa ndimi na viungo vyengine vutamtolea ushahidi mja siku ya Qiyaamah. Asema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Hapa shaka wanaowasingizia**

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

UVUMI NA KHATARI ZAKE

wanawake wanaojihifadhi na zinaa, nyoyo zao zimesalimika, na wenye kuamni (hao wenye kuwasingiziya) wamelaaniwa; wamelaaniwa Ulimwenguni na Akhera na wana adhabu kubwa. Siku zitakaposhuhudia ndimi zao, mikono yao, miguu yao kwa waliyokuwa wakiyafanya (ya mabaya). Siku hiyo atawalipa Allaah hesabu zao kwa haki na watajua yakwamba hapana shaka (Allaah) Yeye ni wa haki uliodhihiri uadilifu wake." [Surat an-Nur:23-25]

Ewe mwenye kueneza uvumi na kutunga urongo! Ewe ambaye usieona raha kuwaona wenye kupendana wakiwa pamoja mpaka wafarikiyane! Ewe muovu ulotopea katika uovu wako! uzuiye ulimi wako kwani ni mwenye kuhesabiwa kwa kila linalokutoka katika mdomo wako. Allaah (سبحانه وتعالى) asema: **"Halitamki neno (mwana-adamu) ila wapo mbele yake Raqeeb na 'Ateed."** [Surat Qaaf:18].

Basi uzuiye ulimi wako na tahadhari na urongo na kueneza uvumi na propaganda, na tahadhari kumtuhumu Muislamu pasi na ushahidi na tahadhari na kumdhania vibaya Muislamu mwenzako. Fikiriya sana!!! Kanakwamba (mimi kwako wewe), ewe masikini siku ya Qiyaamah, siku ya hasara na majuto, amekushika yule ulomdhulumu na huku asema "Umenidhulumu" na huyu mwengine asema, "Umenitukana" na huyu mwengine asema "Umenifanyia Istihzaa'" (shere), na huyu asema "Umenisengenya". Na katika hali kama hii ulokuwa nayo ukawa umeshadho-ofika (ukawa huna nguvu) za kupambana na wote na umenyosha shingo yako ukitaraji usaidizi kutoka kwa Mola wako ili akutoe kutoka kwenye mikono yao ya mashtaka wakati masikio yako yatakaposikiya mwito wa Allaah (سبحانه وتعالى) ukisema: **"Leo italipwa kila nafsi kwa ilichotuma, hapana dhulma leo."** [Surat al-Mu'min:17] ukakumbuka neno lake Allaah akisema: **"Wala usidhanie kuwa Allaah ameghafilika na wafanyayo madhaalim, hapana shaka yuwawapuliziya mpaka katika siku yatakapokodoka mato yao."** [Surat Ibraahim:42]. Twajilinda na Allaah na udhalilifu (siku ya Akhera). Na twamuomba Yeye uongofu na Tawfiq.

SUTRAH

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 4)

"*Iondoe hii pazia yako, kwani mapambo yake yamenishawishi wakati nilipokuwa kwenye swala."* [Bukhaari]

QUR'AAN NA MISWALA (mazulia yenye marembo)

Kuna watu wanaoangika miswala (mazulia) kwenye kuta zao, Aya za Qur'aan, na vitu kadhaa wakiviita kama nakshi za kidini, huku wakidhania kuwa hilo ni jambo la kheri kufanya. Hiyo miangiko yote haifai, isipokuwa kwenye mas-ala machache ambayo tutakayo jaribu kuyazungumza mahali pengine. Kwa dalili hizohizo, hivyo ni vitu vyenye kushawishi na mtu ni lazima aviepuke kuvielekea anaposwali. Suala linalohusiana na jambo hilo ni mazulia yaliopambwa kwa michoro ya nakshi za kiislamu. Huu ndio umekuwa mtindo wa waislamu- mpaka watu wengine wanadhania yakuwa ni lazima waswali juu ya mazulia hayo! Na tumeona watu wengine wakileta miswala yao misikitini na kuitandika juu ya mazulia kuongeza taqwa! Kutumia miswala hiyo kunakhalifu baadhi ya misingi ya kiislamu kama vile:

1. Mazulia hayo yana mapambo ambayo hapana shaka yoyote ni yenye kumshawishi mtu kwenye swala yake.
2. Utumiaji wa mazulia kama hayo ni kukhilafiana na Sunnah ya "Mtume (صلى الله عليه وسلم) na maswahaba zake (رضي الله عنهم) ambao hawakuwahi kutumia vitu vya sanaa kuswalia.
3. Kuendelea kulifanya jambo hilo huleta muigo usio na msingi wa utukufu na umuhimu kwa mazulia hayo kwenye fahamu za watu wajinga.
4. Utumiaji wa mazulia hayo huendelea kumsongeza mtu mbali na ardhi, ambapo Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametuamrisha sisi tujisugue nayo (ardhi). [Saheeha No.1792]
5. Katika misikiti mengi, Imaam huekewa zulia maalum lililotofautiana na yale ya watu wengine. jambo hili humfanya yeye kuwa na hadhi isiyokuwa na msingi wowote katika Uislamu.

PICHA NA MASANAMU:

Uislamu unakataa uumbaji au utengenezaji wa picha na sanamu za wana-adamu, wanyama au vinyago. Jambo hili huwa ni haraam zaidi likihusiana na swala, ambapo vitu hivyo husababisha ushawishi bila ya shaka. zaidi ya hayo, kuzifanya kuwa ndio sutrah au kuzielekea unaposwali, iwapo ni kwa kukusudia au laa, ni mifano ya Ibaadah za masanamu na picha. Na mambo hayo ni kwenda kinyume na misingi ya ujumbe wa Uislamu.

VITU VIFUPI NA MISTARI.

Kuna watu wanaochukua vitu vifupi mno kuwa ni sutrah. Wengine huchora mistari kwenye ardhi, wakitegemea katika jambo hili Hadeeth iliyo dhaeef sana iliyopokelewa na Abu Dawud. Yote hayo ni kinyume na sunnah swaheeh kama tulivyokwisha eleza hapo awali.

RUHUSA YA KUSWALI BILA YA SUTRAH

Mahali pamoja peke yake ndipo inaporuhusiwa kuswali bila ya kuwa na sutrah. Nayo ni hali ya kuswali nyuma ya Imaam. Katika hali kama hiyo, wanavyuoni wanakubali yakwamba mtu hana haja ya kuwa na sutrah, Kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na sutrah na walokuwa wakiswali nyuma yake hawakuwa na sutrah.

KUSWALI NA SUTRAH UKIWA MAKKAH

Sutrah ni waajib ukiwa Makkah kama ilivyo waajib ukiwa nje ya Makkah. Hakuna ushahidi swaheeh wa kupambanua Makkah na sehemu nyengine kuhusiana na suala hili. Wote kina Imaam al-Bukhari na Ibn Hajar wamekwisha eleza udhaifu wa madai yoyote kinyume na hivyo. Kama tulivyokwisha eleza, Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliukita mkuki na kuuelekea aliposwali swala ya Adhuhuri na 'Asr katika bonde la Makkah. Vilevile alivyoingia ndani ya Ka'bah, aliutumia ukuta mmoja kuwa ni sutrah [Bukhaari], na alipoikurubia Ka'bah, aliswali kwa kuifanya maqaam kuwa kati yake na Ka'bah [Muslim]. Hivi pia ndivyo walivyokuwa wakifanya maswahaba zake (رضي الله عنهم) kwa kumfuata yeye (صلى الله عليه وسلم). Anas (رضي الله عنه) aliikita fimbo na akaswali haliyakuwa ameielekea akiwa Masjid ul-Haraam (imepokewa na Ibn Abi-Shaybah kwa upokezi swaheeh), Ibn 'Umar (رضي الله عنه) hakuwahi kumpisha mtu kupita mbele yake alipokuwa akiswali kwenye Ka'bah (imepokewa na al-Fadal bin Dukayn kwa upokezi swaheeh), na hapakuwa na swahaba yoyote aliekhalifiana nao kwenye mas-ala hayo. Ndio Wanavyuoni wakaafikiana juu ya jambo hilo.

UFAFANUZI KUHUSU SUTRAH:

Katika lugha ya kiarabu, neno 'Sutrah' limetokamana na kitendo 'Satara', yenye maana ya kilicho sitiriwa. Kwa hivyo, ni Sitara au'Kivuli' kwa mwenye kuswali. Ni kitu ambacho mtu hukieka mbele yake anaposwali, ili watu wapite ng'ambo yake ya pili wasipate kumkatizia swala yake.

HUKMU YA SUTRAH:

Utumiaji wa sutrah ni jambo la lazima (waajib) juu ya Imaam anaeongoza watu katika swala na vilevile kwa mtu anaeswali peke yake. Hairuhusiwi kuswali pasi na sutrah; na mtu yeyote atakaefanya hivyo kwa kukusudia atakuwa anafanya madhambi. Ikapokewa na Sahl Bin Abi Hatham (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Anaposwali mmoja wenu, ni lazima aielekee sutrah, na ajikurubize nayo- asije shaytaan akamkatiza swala yake."* Nae Ibn 'Umar (رضي الله عنه) akapokea kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema: *"Usiswali isipokuwa uwe umei-elekea sutrah, na wala usimruhusu mtu yeyote kupita mbele yako (baina yako na sutrah). Akitaka kupita kwa nguvu, basi pigana nae kwa sababu qareen wake (shetani wake) yuko na yeye."*

SIFA ZA SUTRAH

UREFU

Urefu wa sutrah ni kiasi cha kiguzo cha kujitegemeza cha kiti kilichoko juu ya ngamia. Talha (رضي الله عنه)akapokea kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa amesema: *"Anapoeka mmoja wenu, kitu mbele yake kinachofanana (kwa urefu) na kiguzo cha kujitegemeza cha kiti kilichoko juu ya ngamia, basi na aswali bila ya kujali chochote kitakachopita kando yake."* Wakati wa vita vya Tabuk, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipoulizwa kuhusu sutrah ya swala, alijibu: *"Ni kama kiguzo cha kujitegemeza cha kiti kilichoko juu ya ngamia."* Wala sutrah na isiwe fupi kuliko urefu huo. Lakini, mtu atakapojitahidi na asifaulu kupata kitu chenye urefu huo, basi atatumia kilicho bora kadiri ya jitihada yake, kama alivyosema Allaah (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa): **"Mcheni Allaah muwezavyo, (mwisho wa jitihada yenu)."** [Surat at-Taghaabun 64:16]

UPANA

Hapana kiwango cha upana au wembamba wa sutrah. Inaruhusiwa kuutumia ukuta, nguzo, mkuki au fimbo, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwahi kutumia vitu kama hivyo, kama tutakavyo zitaja hapo chini.

UMBALI

Ni lazima mtu asimame karibu na sutrah; laa-sivyo, swala yake itakuwa kwenye hatari ya kubatilika. Maelezo hayo yametokamana na maamrisho ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwenye Hadeeth iliyopita, iliyopokewa na Sahl Bin Abi Hathmah (رضي الله عنه). Vilevile, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Mtu anaposwali na kuielekea sutrah, ni lazima aikurubie, hapo Shetani hatoweza kuikatiza swala yake,"* Kwahivyo, mtu hawezi, kwa mfano,kuswali kwenye nafasi ya nyuma ya msikiti akidai eti ukuta wa mbele wa msikiti ndio sutrah yake. Ni lazima ajisongeze karibu nayo, abakishe sehemu kiasi chake ya kusujudu na kiasi cha umbali wa futi moja au mbili (takriban 50cm) zaidi. Hivyo ndivyo alivyokuwa akifanya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama ilivyopokewa yakwamba: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akisimama karibu na sutrah, kiasi ambacho safu baina yake na ukuta ilikuwa ni kipimo cha mikono mitatu kamili." [Bukhaari na Muslim] "Baina ya nafasi ya sehemu aliyokuwa akisujudu Mtume (صلى الله عليه وسلم) na ukuta ilikuwa ni kiasi cha mbuzi kupita." [Bukhaari na Muslim] "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipoingia ndani ya ka'bah, alibakisha takriban urefu wa vipimo vya mikono mitatu baina yake na ukuta kisha akaswali." [Bukhaari] Hivyo basi, yule atakaesimama mbali na sutrah yake zaidi ya urefu wa mikono mitatu (takriban 150cm au 4.6ft) atakuwa amefanya maasia, kwa sababu atakuwa hakuitekeleza amri ya sutrah kama ilivyoamrishwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Mbali na hayo, patakuwa na uwezekano wa kuihatarisha swala yake isikubaliwe kwa kupitiwa na shetani. Kwa upande mwengine, kusimama karibu mno pia si katika Sunnah, na wala mtu asifanye hivyo isipokuwa katika hali ambayo msikiti ukiwa umejaa watu, au akihofia yakwamba watu watapita katikati (baina yake na sutrah yake)

MIFANO KUTOKA KATIKA SUNNAH

Kuna riwaya zilizo swaheeh chungu nzima kuhusu vitu ambavyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivitumia kama sutrah. Kwa mfano, imepokewa yakwamba:

*"Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akitafuta sehemu kwenye msikiti wake yenye kiguzo na kuswali hapo." [Bukhaari]

*"Alipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiswali katika sehemu iliyowazi ambapo hapakuwa na chochote kutumia kama sutrah, huukita mkuki (katika ardhi) mbele yake na akaswali akiuelekea na watu wakiwa nyuma yake." [Bukhari, Muslim na Ibn Maajah]

*"Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akimueka kipando chake (ngamia) kiubavu na akiswali huku amemuelekea." [Bukhaari na Ahmad]

*"Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akikichukua kiti kilichoko juu ya ngamia, akikifunga madhubuti na kuswali akiwa amekielekea nyuma yake." [Muslim]

*"Aliwahi Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuswali akiwa ameuelekea mti".[an-Nasaa'i na Ahmad].

*"Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiswali hali yakuwa amekielekea kitanda ambacho Bibi 'Aaisha (رضي الله عنها) amekilalia (akiwa amejifunika matandiko yake)" [Bukhari na Muslim]

*Pia Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwahi kuswali akiwa ameielekea fimbo, Ngamia na mkeka uliotumiwa kama pazia baina ya vyumba viwili.

*Maswahaba waliwahi kuswali wakiwa wamewaelekea watu waliokuwa wamekaa. Kwahivyo, chochote chenye kutosheleza vipimo vinavyohitajika na ambavyo havitosongea (havito-ondoka) mtu anaposwali vinaweza kutumiwa kama sutrah.

VITU VISIVYOKUBALIKA KUWA SUTRAH:

MAKABURI

Hairuhusiwi kuyaelekea makaburi wakati mtu akiswali, kwani "Mtume (صلى الله عليه وسلم) ametukataza kufanya hivyo pindi aliposema: *"Musiswali haliyakuwa mume-elekea makaburi, na musiyakalie (makaburi) juu yake."* [Muslim]

MAPAMBO

Mtume (صلى الله عليه وسلم) alichukia kuswali akiwa ameelekea kitu cha kumshawishi kwa mapambo, au rangi. Alimwambia 'Aaisha:

(Endelea Katika Ukurasa wa 3)